ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Pili - Tarehe 22 Septemba, 2016

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi na Moja ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi na Moja ya Katiba ya Zanzibar ya 1984.

MASWALI NA MAJIBU

Nam.104

Vitendo vya Unyanyasaji Kwa Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Shamata Shaame Khamis - Aliuliza**:**

Katiba ya Zanzibar inatambua usawa kwa watu wote bila ya kujali jinsia, dini, maumbile ya mtu, asili yake, na kadhalika. Kwa kuwa katika Jimbo la Micheweni bado vitendo vya unyanyasaji kwa watu wenye ulemavu vinaendelea kuwepo jambo ambalo limepelekea kupewa majina tofauti na yale waliyopewa na familia zao lakini pia wazazi wa watoto hao kutokuwapeleka maskuli kwa sababu ya ulemavu wao.

(a) Je, Wizara yako imeshafanya sensa kujua ni watu wangapi wenye ulemavu hapa nchini na ni wangapi wapo mjini na wangapi wapo vijijini.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wazazi na wanajamii kwa ujumla hasa katika Jimbo la Micheweni, ili kupunguza vitendo vya unyanyasaji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 104 lenye vifungu (a) na (b) naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Serikali inaelewa kuhusu vitendo vya unyanyasaji wanavyofanyiwa Watu Wenye Ulemavu sio kwa Jimbo la Micheweni tu bali ni katika maeneo yote ya Unguja na Pemba. Na hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wanaobainika kuhusika na vitendo hivyo viovu ambavyo havikubaliki katika jamii yetu.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa swali lake Nam. 104 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Idara ya Watu Wenye Ulemavu ilifanya sensa ya usajili ya Watu Wenye Ulemavu mnamo mwaka 2011/2012 ili kujua idadi kamili ya Watu Wenye Ulemavu na changamoto zinazowakabili katika maisha yao, ambapo kwa wakati huo idadi yao kwa Unguja na Pemba ilikuwa ni 16,548, hata hivyo tunazo takwimu za kiwilaya kwa mchanganuo ufuatao:-

UNGUJA

- Wilaya ya Mjini kuna Watu wenye Ulemavu 1,363
- Kusini Unguja ni 2,247
- Wilaya ya Kati 1,362
- Wilaya ya Kaskazini “A” 1,865
- Wilaya ya Kaskazini “B” 1,290
- Wilaya ya Magharibi 1,973

Mhe. Spika, kwa upande wa Unguja kuna jumla ya Watu wenye Ulemavu 10,100.

PEMBA

- Wilaya Mkoani 1,442,
- Chake Chake 1,657
- Micheweni 1,680
- Wete 1,669

Mhe. Spika, Jumla ya Watu wenye Ulemavu kisiwani Pemba ni 6,448.

(b) Mhe. Spika, Idara ya Watu Wenye Ulemavu imepanga kutoa mafunzo ya sera, Sheria na Mikataba ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu ili jamii ielewe namna ya kuwapatia haki stahiki Watu wenye Ulemavu na kuondoa Changamoto za kimaisha zinazowakabili ili Watu wenye Ulemavu waweze kuishi kama jamii nyengine, mafunzo hayo yatafanyika katika kila shehia kwa lengo la kuondoa kasoro zinazojitokeza.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mhe. Waziri na ambayo yameonesha mpaka data, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Kwa vile Jimbo la Micheweni ama Wilaya ya Micheweni imeonekana kwamba ipo nyuma kimaendeleo, lakini kutokana na takwimu inayoonesha katika Wilaya za Pemba, inaonekana pia Micheweni inaongoza katika idadi ya watu wenye ulemavu. Je, ni mpango gani maalumu ukilinganisha na hivyo vigezo vya kiumaskini ambavyo vimetawala katika maeneo ya Micheweni kutenga mkakati maalumu wa serikali ili kuona kwamba idadi hii inapungua ili isiweze kuathiri zaidi katika hali hii ambayo ipo sasa hivi ya unyanyasaji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais ningeomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa ujumla Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachukua kila jitihada katika kuimarisha hali ya uchumi kwa nia na dhamira ya kuwaletea maendeleo wananchi wote. Na Serikali inaelewa kwamba yapo makundi maalumu ambayo yanahitaji msaada wa ziada ili wasaidiwe waweze kuishi vizuri zaidi.

Jitihada hizo zinafanywa, lakini kutokana na hali ya uwezo wa kiuchumi tuliyonayo hatuwezi kutoa fungu stahiki kwa ajili ya kuwasaidia wale wote wenye matatizo kama ambavyo mahitaji yapo. Lakini nitoe ushauri tu Mhe. Spika, kwamba sisi viongozi kuanzia ngazi mbali mbali; kuanzia ngazi ya Wadi, Majimbo, Wilaya, Mkoa na Taifa tuna kila wajibu wa kushirikiana na jamii kwa wale wenye nacho kidogo kusaidia wale ambao wapo katika hali ngumu zaidi.

Hata hivyo, tutafanya jitihada mbali mbali kuona namna gani wale wenzetu ambao wapo katika hali ngumu zaidi ili serikali ichukue juhudi za ziada kuwasaidia hawa ambao wameathirika zaidi. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Nimekuona Mhe. Said Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Mhe. Waziri analielewa hili na ametoa takwimu sahihi ya watu wenye ulemavu. Je, ni watu wangapi waliotiwa hatiani kwa kuwanyanyasa walemavu Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mheshimiwa naona ni la kitakwimu lakini jaribu kujibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ijapokuwa sikulisikia vizuri swali lake Mhe. Said lakini ninadhani itakuwa nimeifahamu dhamira yake ni nini.

Mhe. Spika, kama tunavyojua tuna matatizo ya *echo* hapa ndani, na kama hukuzungumza na *microphone* moja kwa moja ni tabu sana kukusikia, lakini acha niendelee kujaribu kama nilivyolifahamu.

Mhe. Spika, ni kweli wapo watu ambao wana mitindo ya kunyanyasa watu wenye ulemavu. Takwimu kamili za watu hao kwa sasa sina lakini nitahakikisha ninamuandikia kwa maandishi ili nimletee takwimu hizo. Lakini jambo ambalo la kusikitisha sana kwamba unaona wenzetu watu wenye ulemavu tayari wameathirika kwa namna moja na bado sisi ambao Mwenyezi Mungu ametupa maumbile kamili, tunafanya vitendo ambavyo haviingii akilini wala si vyema kuvifanya kuwafanyia wenzetu.

Kwa hivyo nitoe wito kwa watu ambao wana tabia hizi tuache mara moja. Na ni vyema tukashirikiana sote hususan jamii inapoona tukio kama hili linatokea katika maeneo yao bila ya kumuonea haya, bila ya kumvumilia kama ni jamaa, rafiki au kwa namna yoyote ile, ili taarifa zitolewe na watu wenye vitendo hivyo hatua za kisheria zichukuliwe ili tukomeshe hawa wanaonyanyasa watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika: Swali la mwisho kwa Wizara hii Mhe. Nadir nilikuona.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi ningeomba kuuliza swali la ziada lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwanza niipongeze sana Serikali, yaani Wizara yake kwa juhudi kubwa inazochukua kusaidia watu wenye ulemavu.

(a) Ni lini wizara yako itakwenda kukaa na wahusika watu wenye ulemavu, viongozi pamoja na wale wengine wenye ulemavu kuwasikiliza matatizo yao.

(b) Kwa kuwa nchi yetu watu wenye ulemavu wengi hawana uwezo hasa wapo watu wazima waliovuka miaka sitini, na wapo waliokuwa chini ya miaka sitini wana upungufu wa baiskeli, wana matatizo wanahitaji miguu ya bandia, mikono ya bandia pamoja na vitu vyengine. Ni lini Serikali kwa hawa wazee waliokuwa miaka hamsini kwenda juu itawapatia hivi vifaa bure.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwanza nipokee pongezi ambazo ametupa kwa namna ambavyo tunasaidia watu wenye ulemavu. Huo ni wajibu wetu.

Kuhusu suala la (a) kukaa nao pamoja.

(a) Mhe. Spika, kwa sababu wao ni sehemu ya Wizara yetu, Idara hii ipo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, suala la kukaa ni endelevu, hukaa kila wakati kutokana na wale Wawakilishi wanachaguliwa kwa niaba ya wenziwao kuzungumzia mambo haya. Na hivi sasa tuna mpango wa kutembelea Wilaya zote kukutana na watu wenye ulemavu ili kusikiliza kwa kina matatizo yao na ziara nitaanzia kwa upande wa Pemba.

(b) Kuhusu kuwasaidia watu wenye ulemavu hasa wenye umri mkubwa kupata vifaa ambavyo vitawasaidia katika kujiendeleza kwa shughuli za kimaisha ya kila siku, zikiwemo baiskeli. Ushauri huu tunaupokea na tulianza kuufanyia kazi na kadri ya uwezo wa nchi utakavyoruhusu basi tutajitahidi kutoa vifaa hivi bure kwa watu wetu hawa. Hata hivyo ningependa nitoe wito kwa viongozi na wale wote ambao wana uwezo, kusaidia jamii ili kuepuka matatizo ambayo yanayowakabili.

Nam. 185

Mafanikio ya Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Aliuliza**:**

Katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Waheshimiwa Mawaziri, na Watendaji Wakuu wa Mawizara, Maidara na Mashirika, wamekabidhiwa Ilani hiyo kwa maelekezo ya utekelezaji wa kazi zao.

Kwa kuwa Ilani ni muongozo wa utekelezaji wa majukumu yao, Je, Mhe. Waziri ni mafanikio gani yamepatikana katika utekelezaji wa Ilani hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) swali lake Nam. 185 naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika**,** nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wa Mawizara, Idara na Mashirika wameshakabidhiwa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015/2020 ili uwe ni muongozo na utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku na kuwarahisishia Viongozi na watendaji hao katika kupanga shughuli zao za utekelezaji.

Mhe. Spika**,** Ilani imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 na mwelekeo ya sera za CCM zenye lengo na nia ya kuendelea kuwatumikia wananchi kwa miaka mitano ijayo 2015 – 2020.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 185 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika**,** mafanikio yaliyopatikana ni mengi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ni mashahidi, Amani na Utulivu inayoendelea nchini ni kielelezo sahihi cha mafanikio hayo. Hali ya ukuaji wa uchumi na ongezeko la huduma za kijamii zinazopatikana nchini kote pia ni uthibitisho tosha cha mafanikio hayo.

Mhe. Spika**,** pamoja na hayo niliyoyaeleza naomba kuyataja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

1. Kuimarika ukuaji wa uchumi wa wastani wa kati asilimia 6 mpaka 7 kwa mwaka pamoja na kuendelea na mkakati wa kupunguza umaskini nchini ili kuongeza kipato cha wananchi wetu.
2. Kuongezeka kwa pato la Taifa kutoka Shilingi za Kitanzania 2,133.5 Bilioni mwaka 2014 hadi kufikia Shilingi 2,308 Bilioni mwaka 2015.
3. Kuimarika usimamizi wa mapato ya ndani kutoka Shilingi za Kitanzania Bilioni 18 kwa mwezi kwa mwaka 2010 hadi kufikia Bilioni 52 kwa mwezi kwa mwaka 2016.
4. Kujenga misingi imara ya kisheria na kisera kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi.
5. Kuimarisha sekta kuu za kiuchumi ikiwemo utalii, kilimo, biashara, uwekezaji na viwanda. Na sasa mkazo umewekwa katika kuhakikisha kwamba tunaimarisha sekta ya mafuta na gesi asilia.
6. Kuimarisha miundombinu mbali mbali ikiwemo barabara, mawasiliano, usafirishaji, nishati, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika.

7. Kuongezeka kwa kasi ya upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya, maji, umeme na kadhalika.

8. Kuendeleza mkakati wa kuimarisha ajira nchini hasa kwa vijana kupitia mpango maalumu wa kuwawezesha wananchi kiuchumi.
9. Kupambana na kila ubadhirifu wa aina zote ikiwemo rushwa na wizi.
10. Kuimarisha sekta binafsi ili iweze kushiriki kikamilifu katika kuimarisha uchumi.
11. Kuhakikisha kwamba tunajenga jamii yenye umoja, upendo, amani na utulivu.

Haya ni baadhi tu ya mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sasa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa taarifa yake nzuri ya kuhakikisha kwamba Chama cha Mapinduzi ndicho kinachoongoza Serikali yetu, na Ilani yake lazima itekelezwe ili mafanikio zaidi yapatikane. Swali

langu liko hapa, Mhe. Spika, uchumi wa nchi ndio maendeleo ya nchi na kusimamia matumizi ni njia moja ya kuleta maendeleo katika nchi, hilo nalipongeza, kukua kwa uchumi na kusimamia vizuri. Swali liko hapa.

Je, kwa kuwa watendaji wengi hawaelewi na hawaielewi ilani ni kitu gani, serikali au wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hawa waliokuwa hawaielewi, hasa sehemu ya Wakurugenzi huku chini, ina mpango gani wa kuwapa taaluma au semina maalumu ili wahakikishe kwamba anapokwenda Mbunge, Mwakilishi au yeyote kudai kazi fulani hasa maji, barabara na mengineyo ajue ni wajibu wake kwamba pale tunatetea Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi itekelezwe, ana mpango gani wa kuhakikisha semina hiyo inafanyika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni utaratibu wa kiserikali kuwataalamisha watendaji wake ili kuelewa umuhimu wa kuwasikiliza wananchi, pamoja na kuwasikiliza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, ili ile dhana ya kutoa huduma bora kwa umma ipatikane.

Hivyo, tutaendelea kuzidi kutoa taaluma na ushauri huo tunaupokea, lakini hivi sasa watendaji wetu wanalielewa hilo. Kwa hivyo, ni wajibu wa watendaji wetu wanapopelekewa malalamiko na viongozi wetu, hususan Wawakilishi wa wananchi, wawasikilize na watekeleze kwa mujibu wa hali ya uwezo wa nchi yetu. Naamini watendaji wetu wana hamu kubwa ya kutekeleza hayo, lakini wakati mwengine wanakwazwa kutokana na uwezo wa kifedha.

Mhe. Spika, suala la msingi hapa ni kushirikiana kuimarisha uchumi wetu, ili tuweze kutoa huduma vizuri zaidi kwa wananchi wetu. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe, kwamba watendaji tutazidi kuwaeleza ili waelewe kwa kina suala hili la kuheshimu maelekezo ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Nimekuona Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tutamalizia na Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri ambaye hana jimbo kwa majibu mazuri, sahihi na muafaka kabisa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu, Ilani ya Chama cha Mapinduzi imefika katika namba saba kuhusu maji na elimu. Je, ni lini wananchi wa Michamvi wataguswa na ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukishuhudia tokea kuanzwa kwa dunia mpaka hii leo hawajapata maji safi na salama, na

ukizingatia kijiji hicho ndiko alikotokea Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu). *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo la *echo* linabaki pale pale, lakini naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim kama nitakuwa nimemsikia vizuri. Naamini dhana nimeielewa, anachotaka kuniuliza ni kwamba, ni lini wananchi wa Michamvi wataiona ilani ya Chama cha Mapinduzi. Naamini wananchi wa Michamvi wanaiona ilani ya Chama cha Mapinduzi. Maana uzuri ni wa barabara ambayo sasa hivi imepita katika eneo hilo la Michamvi. Huko nyuma barabara ile ya Michamvi ilikuwa tabu hata punda kupita, lakini sasa hivi kutokana na ilani ya Chama cha Mapinduzi wana barabara, mtandao wa maji ambao Mhe. Jaku Hashim anakuwa akiusemea sana, tuko mbioni kuhakikisha wananchi pale tatizo la maji linatatuliwa, suala la elimu kwa maana ya skuli zipo Michamvi.

Mtandao ule wa Michamvi pia kuna maendeleo makubwa ya kiutalii, ambayo wananchi wengi wananufaika katika kufanya shughuli zao za kiuchumi, kwa kuuza bidhaa zao mbali mbali katika mahoteli hayo. Naamini yote haya ni kutokana na ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Lakini ile amani na utulivu ya kufanya mambo yao, wajue kwamba hiyo ni sehemu kuu ya ishara njema ya manufaa ya ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Nawaomba sana wananchi wa Michamvi na Mwakilishi wao aone kwamba ilani hii inawafaa wao na itawafaa vile vile vizazi vijavyo, waendelee kuichagua CCM maisha.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya swali mama lililoulizwa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) wa Jimbo la Kijitoupele.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ukiwaacha mawaziri, watendaji wakuu wa wizara, maidara na mashirika, sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuliochaguliwa majimboni, tuna nafasi kubwa vile vile ya utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi. Miongoni mwa mambo yanayotusaidia sana ni Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Nimuulize Mhe. Waziri kwa sababu karibu ni mwezi wa sita huu unaendelea.

Je, ni lini fedha za mfuko wa jimbo zitaingia ili na sisi tuwe na *speed* ya kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi katika majimbo yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza niseme wazi kwamba nimefurahi sana na swali lake, kwa sababu kwanza ameliuliza nimelisikia vizuri, ameweza kukaa na kipaza sauti vizuri kiasi ambacho yote aliyoeleza nimeyasikia.

Pia nashukuru kwa kupongeza utekelezaji mzuri wa ilani ya Chama cha Mapinduzi katika nchi yetu hasa katika majimbo yetu. Nataka nimtoe wasi wasi Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa Wajumbe wote, kwamba wakati wowote kuanzia sasa fedha za mfuko wa jimbo mtazipata, ili mtekeleze shughuli za maendeleo katika majimbo yenu. *(Makofi)*

Nam. 130

Uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: (Kny: Mhe. Shadya Mohamed Suleiman) - Aliuliza:-

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Awamu ya Saba Dkt. Ali Mohamed Shein alisisitiza suala la uwajibikaji kwa wafanyakazi.

a) Je, Ofisi yako imelipa kipaumbele kiasi gani suala la uwajibikaji.
b) Ni wafanyakazi wangapi wameanza kuchukuliwa hatua kwa kutowajibika ipasavyo katika majukumu yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 130 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kwanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein katika hotuba zake mbali mbali, amekuwa akisisitiza suala la uwajibikaji kwa Watumishi wa Umma na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Ninaamini pia kwamba, utekelezaji wa suala hilo unajumuisha mambo mengi na kuhusisha wahusika kadhaa serikalini, ikiwa ni pamoja na viongozi na watendaji wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi, ili waweze kusimamia ipasavyo uzalishaji na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, pamoja na kwamba suala la uwajibikaji linazihusu kila Wizara, Idara,Taasisi,Viongozi na Watumishi wote wa umma, hata hivyo, kutokana na jukumu lake la kusimamia Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inalipa kipaumbele kikubwa suala la uwajibikaji.

   Aidha, katika kuratibu na kusimamia suala la uwajibikaji, ofisi yangu kwa kushirikiana na wizara na taasisi mbali mbali, imeandaa na kutekeleza mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza kuandaa na kusimamia sera, sheria na mipango mbali mbali ya maendeleo na utumishi na kushiriki katika maandalizi na utekelezaji wake.

Miongoni mwa sera na mipango hiyo ni pamoja na:-

i. Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010.
ii. Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010
iii. Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011 na sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa Namba 1 ya mwaka 2012
iv. Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011
v. Sheria ya Maadili ya Viongozi Namba 4 ya mwaka 2015
vi. Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 na miongozo mbali mbali yenye lengo la kufafanua kanuni hizo za utumishi; na
vii. Mipango kazi inayoandaliwa na wizara na taasisi mbali mbali za serikali.

Mhe. Spika, pili kusimamia maandalizi na matumizi ya mifumo mbali mbali ya kiutumishi *(Public Service Systems*) ikiwemo:-

i. Miundo ya kitaasisi kupitia zoezi la mapitio ya majukumu ya taasisi (*Functional Review)*
ii. Miundo ya utumishi kwa kada zote za utumishi wa umma
iii. Miundo ya mishahara na marekebisho yake katika taasisi za umma

iv. Kutoa miongozo kwa ajili ya maandalizi ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja, Mpango wa Rasilimali Watu na Muongozo wa upandishwaji cheo kwa watumishi wa umma.

Mhe. Spika, ufuatiliaji uliofanywa wa utekelezaji wa miongozo na mifumo hii ya kiutumishi, pamoja na mifumo mbali mbali ya kifedha kwa kila kiongozi na watumishi, unadhihirisha wazi kwamba utendaji na uwajibikaji wa wizara na taasisi zetu umeongezeka zaidi.

b) Mhe. Spika, kifungu cha 82 (a) mpaka (c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011, kimefafanua na kuweka mamlaka za kinidhamu, zenye uwezo wa kuchukua hatua kwa watumishi wa umma, ambao hawawajibiki ipasavyo katika taasisi zao. Miongoni mwa mamlaka hizo za nidhamu, ni pamoja na Wakuu wa Maidara na Taasisi, Makatibu Wakuu, Tume za Utumishi, Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe. Spika, kutokana na kuwepo kwa mfumo huo, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria,Utumishi wa Umma na Utawala Bora, haina jukumu la moja kwa moja la kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wasiowajibika katika taasisi zao. Isipokuwa kwa hatua zinazopelekea kuhusishwa mshahara wa mtumishi husika, ndipo Ofisi yangu inapojulishwa rasmi.

Katika hali hiyo, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zimepewa mamlaka ya kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wao wasiowajibika, na kwa hivyo wako katika nafasi nzuri ya kutoa takwimu na idadi yao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo kuhusiana na suala zima la uwajibikaji. Kwa kuwa haki na wajibu ni watoto mapacha na wizara yako inahusika na uwajibikaji wa utumishi wa umma.

Je, ni lini wizara yako itafanya mpango maalumu na utekelezaji wa kuwaondolea matatizo wafanyakazi wanaotoka kwenda kufanyakazi, kutoka Wete kwenda Chake Chake na Mkoani kuja Chake Chake, ili kuwawekea usafiri waweze kuwajibika vizuri, ili fagio hili lisije likawakumba wakaonekana kwamba hawawajibiki, kwa kuchelewa kufika kazini na kuondoka kazini mapema. Ni lini wizara yako itafanya mpango huu na utekelezaji wa kuweza kupatiwa usafiri. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ni kweli kabisa suala la uwajibikaji lipo katika wizara yetu ambapo inasimamia utawala bora na uwajibikaji, ni miongoni mwa misingi ya utawala bora. Kwa hivyo, tatizo ambalo amelisema la kwamba wafanyakazi wanatoka Wete kwenda Chake Chake wanapata tabu, hilo tatizo lipo katika sehemu mbali mbali, lakini kuna mipango mbali mbali serikali imekuwa ikipanga, ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote na sio hao tu wanaotoka Wete kwenda Chake Chake ambao tatizo hili wanalipata, lakini serikali inaendelea kufanya jitihada za makusudi ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi wake pale hali itakaporuhusu kupatiwa huo usafiri, lakini mambo kidogo kidogo, tuvumilie hali halisi ya nchi yetu tunaielewa, lakini *In sha Allah* mambo mazuri hayataki haraka.

Nam. 154

Ununuzi wa Karafuu kwa Madaraja

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa sababu Shirika la Taifa la Biashara hununua karafuu kwa madaraja yaani – Daraja la 1, 2 na 3.

Je, Shirika la Taifa la Biashara (*ZSTC)* kwa Msimu wa Mwaka 2015/2016 lilinunua tani ngapi za Karafuu kwa Daraja la 2 na Daraja la 3.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 154 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) lina jukumu la kununua karafuu zinazozalishwa nchini kwa upande wa Pemba na Unguja. Karafuu hizo hununuliwa kwa madaraja tofauti, yaani daraja la kwanza, pili na tatu kutokana na ubora wa karafuu.

Kwa msimu wa mwaka 2015/2016, Shirika lilinunua jumla ya Tani 5,764.83 za karafuu zenye thamani ya Tzs 80.78 bilioni katika madaraja tofauti. Aidha, karafuu hizo zilizonunuliwa zimegawika katika madaraja matatu kama ifuatavyo:-

Daraja la kwanza - Shirika limenunua Tani 5,736.09 za karafuu zenye thamani ya Tzs 80.44 bilioni sawa na asilimia 99.5

Daraja la pili - Shirika limenunua jumla ya tani 27.25 za karafuu zenye thamani ya Tzs 326.98 milioni sawa na asilimia 0.47

Daraja la tatu - Shirika limenunua jumla ya tani 1.49 za karafuu zenye thamani ya Tzs 165,000 sawa na asilimia 0.03

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, mimi nafurahi na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri aliyoyatoa. Lakini kwa kuwa waziri amekiri kwamba serikali imenunua karafuu kwa madaraja matatu yote katika msimu huu wa mwaka 2015/16, na ametaja shilingi bilioni 80 ambazo zimetumika. Sasa ukizifanyia hesabu, hesabu yake aliyoisema inaingia hata kama itanunuliwa kwa daraja la kwanza zote zinazidi shilingi 14,000. Je, haoni kwamba hesabu hizo zitakuwa zimepingana na maelezo yake waziri.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mhe. Spika, kwa kweli sijamuelewa swali lake, kwa sababu swali lake aliuliza tani ngapi tumenunua na kwa *grade* zipi. Mimi nilimjibu karafuu tulizonunua na madaraja yake. Sasa kama anaona hesabu zimepungua, kwa sababu kuna manunuzi ya makonyo vile vile hayakutiwa humu, kwa sababu hamkuniuliza masuala ya makonyo. Kwa hivyo, bei hii ni kwa ajili ya karafuu zilizonunuliwa kipindi kile, kwa hivyo hesabu ni sawa sawa Mhe. Spika.

Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo): Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa na mimi nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifutavyo:

Mhe. Waziri kule Bara idadi ya watu ni kubwa na wengi wao ni masikini lakini wanatumia bidhaa nzuri na zenye ubora kama vile mchele wa Mbeya, Kyela na mafuta ya kupikia. Je, Wizara yako ni lini itatoa elimu kwa wafanyabiashara wa Zanzibar ambao wanaingiza bidhaa ambazo hazina ubora kama vile mchele wa mapembe.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika suali lililoulizwa lilikuwa ni karafuu, lakini nitamjibu kwa ajili ya kuwaelimisha na wananchi. Hata Zanzibar vile vile Mhe. Spika, tunakula vyakula vyenye viwango kwa sababu vyakula vyote vinavyoingizwa nchini vinatakiwa vitimilize viwango vilivyowekwa sawa sawa na Serikali kupitia chombo chetu kinachoangalia ubora wa vyakula na viwango, lakini pia tuna chombo chetu sisi cha kuweka ubora, cha *Zanzibar Bureau of Standards;* na vile vile kukitokea

hitilafu nao wanashirikishwa kuhakikisha kwamba bidhaa zinazoingia ni za ubora.

Suala la mapembe niliwahi kulitolea ufafanuzi kwamba mapembe sasa hivi tunataka mapembe ambayo hayajakaa muda mrefu, vyakula vilivyokuwa havijakaa muda mrefu kwenye maghala tatizo kubwa linalokuja hapa Zanzibar ni kwamba bei ya vyakula tunavyovitaka ambavyo vya masokoni vinavyozalishwa kipindi cha mwaka huu, kwa mfano inakuwa ni kubwa sana, wananchi wengi wao hawawezi kununua vyakula vya aina hii, na ndio maana hapo nilipopenya wafanya biashara wakaona kwamba bora wanunue vitu ambavyo vilivyokuwa bei nafuu kidogo ili wananchi wengi waweze kujihudumia.

Lakini tumeamua kuweka tarehe maalumu kwa ajili ya vyakula vinavyoagizwa hasa mchele tarehe ile isipindukie ili mchele unaokuja Zanzibar uwe wa uhakika, sasa hivi tunawaelekeza wafanyabiashara kwa mfano mchele wanunue nchi ambazo tuna mawasiliano nao vizuri, kwa mfano wamekuja watu wa Vietnam na tunawashawishi sana wafanyabiashara waende wakanunue vyakula vyao kama hivyo Vietnam, kwa sababu hata Serikali ya China wananunua sehemu kubwa ya mchele sasa hivi kutoka Vietnam.

Lakini niwahakikishie tu kwamba vyakula vinavyokuja Zanzibar sehemu kubwa navyo vina ubora mzuri, kwa sababu Serikali inasimamia ubora na kulinda afya za wananchi wake.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, zao la karafuu ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu na kwa asilimia kubwa tunalitegemea ili tupate shughuli zetu mbali mbali ziendelee vizuri kwa maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar. Swali langu lipo hapa, pamoja na kujibu maelezo yake mazuri kwamba zimenunuliwa karafuu katika madaraja matatu la kwanza, la pili na la tatu lakini inasemekana katika kipindi chenye udanganyifu mkubwa wa kuchanganya madaraja badala ya lile la tatu na pili kuwa la kwanza, hilo linasemekana lipo, na kuna watu wanatoa malalamiko yao kwa kuwa wanatupenda baadhi ya watu katika nchi yetu.

Je, Mhe. Waziri hili amelifanyia uchunguzi kiasi gani na amegundua vipi na mimi niliyesimama hapa haya ninayosema nasema kwa uthibitisho, kwamba watu wako tayari kutoa maelezo, atakuwa tayari Mheshimiwa kufuatana na mimi kwenda kwa hao watu wanaohusika juu ya udanganyifu huu unaofanyika.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Suala la udanganyifu wakati wa kuuza karafuu na kuchanganya karafuu na kudai kwamba ni *grade* ya juu hilo jambo lilikuwepo, nakubali kwamba lilikuwepo lilikuwa likitokea sana hasa Pemba sana yakitokea matatizo haya.

ZSTC na Wizara yetu imejitahidi kupunguza kesi kama hizo za kuchanganya karafuu na kusema kwamba hizi ni za *grade* ya kwanza, na tuliona kwamba mambo haya yalifanyika baadhi kati ya mashirikiano ya wale waliokuwepo kwenye vituo, kunakuwa na watendaji wa Wizara ya Kilimo na watendaji wa *ZSTC* hapa kunakuwa na mchezo, au siku hizi wanasema michongo ndivyo ilivyokuwa inafanywa.

Kwa hivyo kuondosha tatizo hili sasa hivi nafikiri baada ya siku tatu nne tutapata mashine za kusafishia karafuu tumepewa msaada na watu ambao tunawauzia karafuu, kwanza kuzisafisha na kuzileta Zanzibar na kuuzwa karafuu safi kwa mujibu wa *grade* yake. Kwa sababu huu mchanganyo uliokuwa unafanya kati ya karafuu na nyunga mbali mbali umesababisha karafuu za Zanzibar kuporomoka katika soko kwa sababu karafuu za Zanzibar zilizouzwa kiholela kama hivyo zimeharibu kabisa sifa ya karafuu ya Zanzibar, kwa hivyo sasa hivi Wizara iko macho sana, na mashine hizo ambazo tutaanza kuzitumia msimu unaokuja zitasaidia sana hasa udanganyifu wa aina hiyo kuwa hawapo, ila sasa hivi unapokwenda kuuza karafuu hazichukuliwi mpaka uzimwage mwenyewe mnunuzi, halafu unazipeleka pale pale kituoni karafuu ambazo zinakidhi kiwango.

Nam. 88

Kukosekana kwa Huduma ya Chakula kwa Wagonjwa Hospitali ya Micheweni

Mhe. Shamata Shaame Khamis - Aliuliza**:**

Katika kipindi cha nyuma Hospitali ya Wilaya ya Micheweni ilikuwa ikitoa huduma ya kuwapatia chakula wagonjwa wanaolazwa hospitalini hapo, jambo ambalo husaidia kurahisisha matibabu kwa wagonjwa, kwa sababu wanakula kwa wakati na pia wagonjwa hufarijika, lakini ni muda mrefu sasa huduma ya chakula kwa wagonjwa hospitalini hapo haipatikani.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea kusitishwa kwa huduma hii katika Hospitali ya Micheweni.

(b) Je, Wizara kusitisha huduma hii haioni kuwa ni kuwazidishia maradhi wagonjwa wanaolazwa hospitalini hapo ikizingatiwa kuwa wagonjwa wengine wanaolazwa hapo huwa wanatoka maeneo ya mbali na jamaa zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, huduma ya utoaji wa chakula katika hospitali zetu za Serikali ni moja ya huduma ambayo inazingatiwa kwa kiasi kikubwa na Wizara ya Afya ingawa ufanisi wake hutegemeana sana na upatikanaji wa fedha. Ni kweli baadhi ya wakati chakula cha wagonjwa kilikuwa hakipatikani, hali hii ilichangiwa na ufinyu wa bajeti kwa huduma za afya na pia uwepo wa maradhi ya kipindupindu kwa muda mrefu takribani mwaka mzima, hali hii nayo ilichangia kwani fedha nyingi zilielekezwa katika kudhibiti maradhi ambayo yamegharimu fedha nyingi ambazo zingetumika kwa masuala mengine ikiwemo kununua chakula cha wagonjwa.

(b) Mhe. Spika, bado huduma ya utoaji wa chakula katika hospitali ya Micheweni haijasitishwa kwani hii ni huduma endelevu. Kuanzia mwezi Juni, 2016 hadi leo huduma hii inaendelea kutolewa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mhe. Shamata Shaame Khamis: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza Mhe. Waziri.
Kwa vile amekiri kwamba ufinyu wa bajeti na sababu nyengine ambazo amezitaja kwamba zimekuwa zikichangia huduma hii isiende kama vile ambavyo imekusudiwa, lakini bado nimuulize Mhe. Waziri.

Ni lini Serikali yetu kwa kupitia Wizara hii itakuwa na mpango kabambe wa kuona kwamba suala hili halikatishwi katishwi ukilinganisha na hali za wagonjwa wetu wanapofika pale hospitalini hususan katika wilaya ile, ni kwamba mtu anaweza kutoka sehemu husika akafika pale akawa hana mtu wa kumsaidia, kwa hivyo nataka kupata majibu kwa kupitia swali hili dogo. Ahsante sana Mheshimiwa

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mheshimiwa Wizara ina mpango madhubuti wa kuona hali hii haijirudii kwa kuhamasisha katika hospitali na vituo vyetu kuwa na *basket fund,* mfuko huu ni mfuko maalumu kama utakubalika vizuri katika

hospitali zetu, kwa sababu washughulikiaji wa mfuko huu kamati zetu za maendeleo na kamati za afya.

Mara nyingi tunapofanya ziara katika vituo na hospitali zetu tunahamasisha mfuko huu uchangiwe, kwa sababu ya kuhudumia huduma ndogo ndogo na kubwa kubwa ambazo ni za *emergency* zinazojitokeza, tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi mutusaidie kuhamasisha kukutana kwa vikao vya kamati hizi za Afya, kamati za Majimbo, pamoja na kamati zenu Waheshimiwa Wawakilishi ili kudumisha mifuko hii ambayo inaweza ikasaidia katika matatizo yanayojitokeza mara moja.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri amesema chakula kinatolewa lakini hali ni mbaya, na amewataka Waheshimiwa Wawakilishi na mifuko ya maendeleo wachangie, lakini Wawakilishi hao wanatakiwa wachangie madawati, wanatakiwa wachangie njia, sasa mpaka kiingie na chakula cha wagonjwa hospitali sasa swali langu liko hapa.

Ni kiasi gani Serikali imetenga kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya chakula cha Wagonjwa katika hospitali zetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Naomba radhi takwimu sahihi sina sasa hivi lakini nitaileta kwa maandishi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kuweka huduma ya *x-ray* katika hospitali ya Micheweni, swali langu ni dogo sana, je, ni wafanyakazi wangapi wa *x-ray* wamepelekwa Micheweni ili kuendeleza huduma hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwa kipindi kirefu kulikuwa hakuna mfanyakazi wa *x-ray* katika hospitali ya Micheweni, lakini kwa sasa Wizara imeandaa mfanyakazi mmoja wa kufanya huduma ya *x-ray* Micheweni na mwengine anakwenda na kurudi kwa siku maalumu, lakini mmoja ambaye ni mfanyakazi na mkaazi wa Micheweni yupo anaandaliwa kwa ajili ya kutoa huduma hiyo.

Nam. 39

Kukosekana kwa OB VAN Katika ZBC

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Mashirika mengi ya Habari duniani, wakiwemo jirani zetu TBC wanakuwa na OB VAN kwa ajili ya kurushia matangazo katika maeneo mbali mbali.

(a) Je, sababu zipi zilizopelekea ZBC –TV kutokuwa na *OB VAN*.
(b) Je, Serikali haioni haja ya kuwa na chombo hichi cha *OB VAN* katika Shirika letu la ZBC – TV.
(c) Je, Serikali haioni kuwa kutokuwa na *OB VAN* pale ZBC – TV itashindwa kuhimili ushindani wa vyombo vya habari hasa katika kipindi hichi cha ukuaji wa Tasnia ya Habari na Mawasiliano.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 39 lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli ZBC TV kwa sasa haina *OB Van* na sababu zilizopelekea kutokuwa na *OB Van* ni kuchakaa kwa *OB Van* la zamani na bado halijanunuliwa jengine.

b) Mhe. Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi juu ya umuhimu wa kuwa na *OB Van*, Serikali inakiri ipo haja ya kuwepo *OB Van* ZBC na suala hilo limo katika mipango yake ya baadaye, hilo *OB Van* litanunuliwa hali ya fedha itakaporuhusu

c) Mhe.Spika, kutokuwepo kwa *OB Van* kunaweza kupunguza ufanisi, lakini kutokuwepo kwa *OB Van* sio sababu ya kutoweza kuhimili ushindani wa vyombo vya habari, kwani kazi zinazofanywa na *OB Van* zinaweza zikafanyika kwa njia nyengine ambapo hata hili Baraza lako Tukufu la Wawakilishi linarushwa kwa namna hiyo.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza kama ifutavyo.

Kwa kuwa kuna mpango wa kuliimarisha Shirika letu la ZBC kwa kulipatia mitambo na vifaa vya kisasa, je, ni lini mpango huo utaanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Lengo la Serikali ni kuiboresha sekta hii ya habari kupitia Televisheni ya Taifa, kwa hivyo nimwambie Mhe. Mwakilishi sasa hivi Serikali kupitia Wizara ya Habari imo katika mchakato wa kuboresha sekta hii na tumo katika utaratibu wa kukitafuta hichi kifaa ili tuone kwamba Wizara imeboreka kwa kutoa habari nzuri. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri ZBC ni mdomo wa Serikali ya Zanzibar, na TBC ni mdomo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini ZBC haionekani kwenye ving'amuzi mpaka ulipie, TBC inaonekana bila ya malipo.

Je, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba ni kuwanyima haki wananchi wa Zanzibar wanapoikosa huduma hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Nakubaliana na yeye kwamba ZBC TV au chombo cha habari ni mdomo wa Serikali, na nakiri kwamba ving'amuzi kwa upande wa Zanzibar bado havijakuwepo sahihi, lakini nimuahidi kwamba kupitia swali lake hili najua kwamba ni ushauri anataka tuboreshe chombo hichi cha habari kupitia ZBC TV, namuahidi kwamba Serikali imo katika mipango ya kuiboresha hii sekta kwa kutafuta ving'amuzi ili wananchi waendelee kufaidika na wala haina lengo la kutowatendea haki wananchi wake wa Zanzibar.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza:

Hoja ni kwamba Zanzibar kuna ving'amuzi kwa mfano kama AZAM na ving'amuzi vile na vyenginevyo ving'amuzi vile ZBC haionekani, sasa *point* ni kwamba hivi ving'amuzi vinavyokuja Zanzibar na vinavyosajiliwa kitu kimoja waambiwe lazima *domestic television* ya Zanzibar iwe inaonekana. Kwa sababu ZBC ndio mdomo wa Serikali ndio inayo- *disseminate* sera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sasa nauliza lini hivyo ving'amuzi vyengine vyote *ZBC* itaonekana.

Mhe. Waziri wa Habari Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu wa Jimbo la Welezo pamoja na ziada ya Mhe. Suleiman, kwa suala lililopita. Kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa majibu yake

mazuri kabisa aliyoyatoa na ambayo yako kwenye mstari kabisa. Napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba kwa hivi sasa *ZBC* inatangazwa kupitia ving'amuzi. *ZBC* ina king'amuzi chake ambacho kinaitwa *TING*. Kwa hivyo, kwa wale ambao wamenunua king'amuzi cha *ZBC, ZBC* kwanza inaonekana kwenye king'amuzi chake *TING*. Yaani Tanzania *Integral Network Group*. Lakini vile vile *ZBC* inaonekana kupita ving'amuzi vyengine. Mwenye king'amuzi cha *ZCTV, Zanzibar Cable Television,* inaonekana, kwenye king'amuzi cha *AZAM* inaonekana, kwenye *Star Time* inaonekana. Hapa inaonekana kwamba kila anayenunua king'amuzi kile televisheni ile anapaswa kuiona. Sasa ni sera na taratibu za sheria ambazo tunaweza kuziweka sisi hapa kupitia Shirika la Utangazaji kuweka sera ambazo zinatumika kimataifa, kwamba Televisheni ya Taifa ni lazima ionekane bure kwenye ving'amuzi vyote ambavyo vitakuja kwenye kuonesha televisheni zake Zanzibar.

Nataka niwaahidi Waheshimiwa Wawakilishi, kupitia Baraza lao taratibu hizi zipo, tunaendelea kudumisha taratibu za matangazo, *productions* zetu ziwe safi. Kwa sababu haitawezekana kama *productions* zetu hazijaingia katika ushindani halafu sisi tukaonekana kwamba leo tunaonekana kwenye king'amuzi kesho tumetoka. Hata hao tutakaoingia nao mkataba tutakuwa hatuko katika pahali pazuri. Nataka niwahakikishie kabla ya Disemba hali nzuri ya Televisheni ya Zanzibar wataiona na ving'amuzi vyote iwe *ZCTV*, iwe *AZAM*, iwe *Star Time* na yeyote atakayekuja kutangaza matangazo yake Zanzibar atapaswa kwanza kuingiza Televisheni ya Zanzibar ndani ya king'amuzi chake.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, samahani maana yake ninapata *note* hapa kuna wajumbe hawajui *OB VAN* ni kitu gani, imejibiwa kwenye swali lakini hamkufafanua ni kitu gani.

Mhe. Waziri wa Habari Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, *OB* ni neno la ufupi; O maana yake *outside* na B maana yake *broadcast,* kwa kirefu *Outside Broadcast* ni yale matangazo yanayotangazwa *live* nje ya kituo. Kwa mfano hapa Mheshimiwa, kituo chetu kipo pale *Karume House*, lakini Baraza lako Tukufu linaonekana *live* nje ya kituo. Hapa chombo kinachotumika inawezekana ikawa *OB VAN* au aina nyengine ya chombo kama hicho. Hapa tunatumia *up link* kwa kuweza kurushia matangazo yetu, hatupitii kwenye *OB VAN*. Lakini kuna vyombo mbadala kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri, kwa mfano *fly way link.* Sasa *fly way kits* sasa hivi zinatumika badala ya *OB VAN.* Nataka kuwafahamisha waheshimiwa wajumbe suala la *OB VAN* ni suala la kizamani kwa mtindo wa kisasa na Zanzibar inavyotaka kuelekea kwenye hii *digital* tutatumia vyombo vinavyoitwa *fly way kits.* Hivi ni vifaa ambavyo unaweza kubeba mgongoni, ukimuona leo Mhe. Mwakilishi kenda

kwenye Jimbo papo hapo unamuonesha kwenye televisheni *live,* lengo la vyombo hivi ni kuonesha *programmes* zetu *live*. (*Makofi*)

Nam. 82

Watu wenye Ulemavu wa Uziwi kukosa Taarifa

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Aliuliza:-

Suala la kupata habari ni suala muhimu kwani kila mmoja wetu anahitaji kupata taarifa zinazohusu mambo mbali mbali ya nchi yake, tukizingatia kwamba nchi yetu inaheshimu misingi ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora.

Serikali haioni kwamba inakiuka misingi hiyo kwa kutowatendea haki watu wenye ulemavu wa uziwi kwa kukosa mawasiliano katika vyombo vya habari hasa televisheni kwa kushindwa kuajiri wakalimani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis swali lake namba 82 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendeshwa kwa misingi ya sheria na haki za kibinaadamu na wala haibagui jamii yoyote, kupitia Shirika la Utangazaji *ZBC*, halikiuki na wala halitokiuka misingi ya kuwanyima habari wananchi wake na hasa Walemavu wa kutokusikia kwa kukosa mawasiliano katika vyombo vya habari hasa Televesheni, kwani *ZBC*, imeweka mkalimani wakati wa taarifa ya habari ambaye huwasiliana kwa lugha ya ishara kwa dhamira ya kuwapasha habari watu wenye ulemavu wa aina hiyo.

Mhe. Spika, vile vile, kwa kutambua umuhimu wa watu wenye ulemavu wa kusikia Shirika la *ZBC* wakati wa kutangaza shughuli za Baraza la Wawakilishi humshirikisha mkalimani kwa lengo la kutafsiri hoja, mijadala na matukio yote muhimu yanayoendelea katika chombo chako hiki muhimu cha Baraza la Wawakilishi nchini.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza, kabla sijauliza swali la nyongeza, kwanza ningeomba nielekeze kutokana na majibu wa Mhe. Naibu Waziri, ametumia neno ambalo wenyewe watu wenye ulemavu hawapendi kutumia. Wale Mhe. Naibu Waziri, wanaitwa viziwi, wasiosikia ni wale watu watukutu ambao hata mtu mwenye masikio yake anaweza akawa hasikii.

Swali langu la nyongeza Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, je, mpaka sasa wizara ina mikakati gani ambayo iliyochukua kuhakikisha wanafanikisha hiyo mipango ambayo wameipanga.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza niombe radhi kwa neno ambalo limefanyiwa marekebisho. Kwa sasa hivi wizara imejipanga kwa kuwatafuta wafanyakazi au watu wenye ulemavu hawa kwamba ionekane na wao wana uwakilishi wao pale katika kuzipata hivi habari kwa kupitia taarifa ya habari na sehemu nyenginezo. Hii kwa sasa hivi nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba, tayari sasa hivi tumo kwenye mchakato na tumeshawatafuta watu wawili pale wakati wowote wataajiriwa na pia wataonekana kwa sababu ukilinganisha na hali yetu ya Ofisi, kilichotukuza kidogo sasa hivi ni ile sehemu ya kusomea taarifa habari kwamba hawaenei watu watatu mpaka wanne kwa wakati mmoja. Kwa hivyo, hili niwambie kuna kitu tunakirekebisha sehemu ya kukaa yule mtu anayeonesha ishara hii ya watu wenye ulemavu, yaani viziwi na ikikamilika nimuahidi Mhe. Mwakilishi, si muda mrefu ataona kwamba na wao wanathaminiwa. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwanza mimi niwapongeze sana wakalimani kwa kazi ngumu wanayoifanya, lakini kumekuwa na harufu kipindi kilichopita kuhusu maslahi yao kama wizara yao maslahi yakoje, wakalimani hao wanaofanya kazi ngumu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, maslahi ya wafanyakazi wote Zanzibar au na kwa mataifa mengine kuna taratibu za kiutumishi ambazo zinatuongoza. Kwa hivyo, nimwambie Mhe. Mwakilishi, kuwa hawa maslahi yao tutaangalia pale palipo na haja ya kutengenezewa maslahi yao tutawashughulikia na tutahakikisha kwamba na wao wanapata maslahi yao kama wanavyostahiki.

Nam. 25

Kupandishwa Kodi kwa Wananchi Wanyonge Wanaoishi Nyumba za Maendeleo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa Muasisi wa Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964 Sheikh Abeid Aman Karume aliona mbali na kuasisi ujenzi wa nyumba za makaazi kwa wananchi wanyonge masikini wakae kwenye makaazi bora na siyo kwenye

vibanda. Na kwa kuwa hivi sasa nyumba hizo zipo chini ya Shirika la Nyumba ambalo limekuwa likipandisha kodi kila baada ya muda kwa wakaazi wa nyumba hizo. Na Kwa kuwa wananchi wanasumbuka na kuumia kutokana na ongezeko hilo la kodi kila mara.

a) Je, kuwapandishia kodi wananchi wanyonge masikini wanaokaa nyumba hizo, na kuwafanya washindwe au wahangaike kulipa ni sawa na kudhihaki na kukejeli dhamira njema na nia nzuri ya Muasisi wa Mapinduzi Sheikh Abeid A. Karume ya kuwapa makaazi bora wananchi bila usumbufu.

b) Kupandisha kodi bila kuzingatia upandaji wa gharama za maisha, si sawa na kurudisha nyuma, ari na sera nzuri ya waasisi za kudumisha malengo ya Mapinduzi ya kujali wananchi wanyonge.

c) Serikali haioni kuwa kadri inavyoacha Shirika lijikite kufanya biashara tu na kutojali asili ya sera ya makaazi, ni sawa na kuwafanya wananchi wadharau Mapinduzi yao matukufu kwa kuona malengo yake yanapuuzwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje swali lake namba 25 lenye vifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Muasisi wa Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964, Sheikh Abeid Aman Karume, aliona mbali na kuasisi ujenzi wa nyumba za makaazi kwa wananchi wanyonge, masikini ili wakae kwenye makaazi bora na siyo kwenye vibanda.

Ni kweli pia kuwa hivi sasa nyumba hizi ziko chini ya Shirika la Nyumba lililoundwa kwa makusudi kuendeleza azma na nia njema ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kuwapatia wananchi wake makaazi bora na kuendeleza ujenzi wa majengo ya kisasa ili kuongeza haiba ya mji katika nchi yetu kwa ajili ya kukuza maendeleo na ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Shirika la nyumba la Zanzibar limeundwa kwa sheria nambari 6 ya mwaka 2014 na kuanza kazi zake rasmi kuanzia Septemba 2015, tangu kuanza kazi Shirika hili limepandisha kodi za nyumba zake mara moja kuanzia mwezi wa Machi, 2016, hivyo basi, naomba iondoke dhana kuwa Shirika limekuwa likiongeza kodi mara kwa mara hivyo kuleta ufumbufu kwa wananchi. Majibu ya maswali ya msingi aliyouliza Mhe. Jaku, ni kama ifuatavyo:-

a) Dhana ya kuongeza kodi ya nyumba hizi ni kuliwezesha Shirika la Nyumba Zanzibar kuweza kuanza kuzifanyia matengenezo ya lazima nyumba hizi ambazo kutokana na hali ngumu ya kifedha inayoikabili Serikali kwa muda wa miaka mingi sasa nyumba hizi zimeachwa bila ya kufanyiwa matengenezo ya lazima. Ongezeko la kodi lililofanywa na Shirika la Nyumba limezingatia hali halisi ya nyumba hizo pamoja na namna ya wapangaji wake ndio maana kiwango chake hakikaribii viwango vya kodi vya wapangishaji wengine wa nyumba kama hizo hapa Zanzibar. Ni mategemeo yetu kuwa wananchi watakuwa pamoja na Serikali katika nia yake ya kuzitunza nyumba hizo kwa kuzifanyia ukarabati stahiki ili zidumu na kunufaisha vizazi vijavyo. Gharama za matengenezo ya nyumba hizi hazina budi kutoka katika kodi za wapangaji wake, hivyo, mchango pekee kwa wananchi wanaotumia nyumba hizi ni kulipa kodi walizopangiwa tena kwa wakati.

b) Kama nilivyoeleza katika majibu ya swali (a) hapo juu, Shirika limezingatia sana upandaji wa gharama za maisha zinazotokana na upandaji wa bei za bidhaa za mlaji pamoja na bei za vifaa vya ujenzi na kuweka kodi ambayo iko chini sana kuliko kodi za chumba chochote cha kawaida katika maeneo hata ya nje ya mji wa Zanzibar. Ni wajibu wetu kama Waheshimiwa kwa kushirikiana na Serikali kuwashajiisha wananchi wetu kurudisha ari ya ujenzi wa taifa kwa kila mmoja wetu kulitumikia Taifa lake kulingana na nafasi aliyoko.

   Ari na sera nzuri ya kudumisha malengo ya Mapinduzi matukufu ya Januari, 1964 yaliwezesha kufanikisha ujenzi wa nyumba za maendeleo mjini na vijijini kwa mashirikiano makubwa na moyo wa kujitolea uliokuwa ukionyeshwa na wananchi wa Zanzibar kwa wakati huo kufikia hadi watumishi wa Serikali kukatwa sehemu ya mishahara yao na wananchi wa kawaida kupangiwa siku maalum za ujenzi wa Taifa katika sehemu mbali mbali ikiwemo ujenzi wa nyumba hizi.

c) Dhana na dhamira ya Serikali kuunda Shirika la Nyumba Zanzibar ni kujenga uwezo wa kifedha na kitaasisi katika kuratibu kwa namna bora zaidi na kwa kuzingatia mazingira na hali ya uchumi wa nchi juu ya kufikia malengo ya Mapinduzi Matukufu ya kuwapatia wananchi wake makaazi bora.

Lengo la Mapinduzi matukufu ya Januari, 1964, ni kuwapatia wananchi wote wa Zanzibar makaazi bora. Idadi ya wananchi wanaofaidika na nyumba za

maendeleo zilizoweza kujengwa Unguja na Pemba baada ya miaka 52 ya Mapinduzi hayo ni sehemu ndogo tu ya wananchi wa Zanzibar. Kwa kipindi kirefu sasa Serikali kutokana na hali ngumu ya kiuchumi haijaweza kufanya ujenzi mkubwa wa majengo ya makaazi ili kutoa fursa ya makaazi bora kwa idadi kubwa ya wananchi waliobaki. Kwa kuzingatia hayo, ndipo Serikali ikaunda Shirika na kulipa mamlaka ya kuendeleza sekta ya nyumba kwa njia ya kibiashara ili kuhakikisha kuwa nyumba zilizojengwa zinadumu na pia kujenga nyumba nyengine kwa ajili ya wananchi wake.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako hili Tukufu naomba sana waheshimia wajumbe wa Baraza hili kuendelea kutoa elimu hii kwa wananchi wetu ili waungane na Serikali yao katika kufikia malengo ya kuwapatia makaazi bora wananchi wa Zanzibar kama yalivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015/2020 na kama ilivyoainishwa katika malengo ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Pamoja na kuenzi dhamira njema na nia nzuri ya Muasisi wa Mapinduzi yetu Sheikh Abeid Amani Karume. Inawezekana tutimize wajibu wetu. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili yenye kifungu (a) na (b).

(a) Nyumba nyingi Mhe. Naibu Waziri, zinakabiliwa na uchakavu, nani mwenye dhamana kati ya mpangaji na Serikali na huku tukishuhudia nyumba hizo nyingi zinafanyiwa matengenezo na wapangaji. Kumekuwa na utaratibu wakenda kudai kule kumekuwa na usumbufu kwa gharama zile. Vile vile, kuna nyumba nyengine tayari zimeshaanguka, Serikali haina uwezo wa kuzijenga na nyinyi hamtaki kuziuza imekuwa ni sawa sawa na nyoka wa mdimu kuzuia kitu wakati hana kazi nacho. Mnatoa kauli gani kuhusu suala hilo.

(b) Tangu kuundwa kwa Shirika hilo kiasi gani cha mapato kimepatikana ukilinganisha na huko nyuma ili wananchi wapate kujua kuanzishwa kwa Shirika hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo Shirika la Nyumba limeanzishwa ili kutatua hili tatizo alilolisema kwamba nyumba nyingi hizi zilikuwa chakavu hata vile vile utakuta kwamba miundombinu yake vile vile imekuwa chakavu. Nampa mfano mmoja tu mzuri, kuna majengo yetu kule ya maendeleo ya Kengeja ambayo majengo yale yako katika hali mbaya sana na gharama za

kuweza kulikarabati tena jingo lile linahitaji pesa zaidi ya shilingi bilioni tatu, ukiangalia si pesa kidogo, ndio maana sasa Shirika limeundwa na kulipa uwezo kwa mujibu wa sheria hii ambayo Ibara namba 7 kuanzia kifungu namba 1 mpaka 4 kinaelezea majukumu yake yote. Akiifungua sheria hii Mhe. Jaku, atakuta hayo majukumu aliyoyauliza ambapo sheria hii imeipa haki Shirika la Nyumba kufanya ukarabati na vile vile, iwapo mwananchi yeyote atafanya ukarabati basi ukarabati huo iwapo utaenda kinyume na taratibu zetu basi tuna wajibu wa kumpiga *fine* kuanzia laki tano mpaka milioni mbili na vile vile, kuurejesha uhalisia wa ile nyumba aliyoifanyia ukarabati ikiwa haiendani na viwango au zile taratibu tunavyotaka.

Swali laki la pili, ameulizia kuhusu hizi nyumba mbovu ni kweli hilo hilo kwa sababu kauliza (a) na (b) hapo hapo na baadae kachomekea (c). Ni kweli kama tunajua wazi kuna nyumba nyingi mbovu katika Mjimkongwe tu peke yake kuna nyumba 12 ambazo tumezitembelea sisi zikiwemo za pale Mchambawima Shangani zinakaribia kuanguka. Gharama za kujenga nyumba iliyoanguka ni kuwa sana, lakini sisi tunalijua hilo ndio maana tukaanzisha hili Shirika la Nyumba. Nina imani kubwa sana mkitupa muda basi hili Shirika la Nyumba litafanya mambo mengi tu mazuri na nina imani sana na Shirika hili la Nyumba kupitia watendaji wake.

Swali lake la (c) ambalo yeye alisema (b) ni kwamba tokea tuanze kukusanya madeni kuanzia Januari, 2016 mpaka Machi, tulipoanza kupandisha hizi kodi mpaka hivi sasa tushakusanya zaidi ya milioni mia nne na sabiini na tatu elfu. Kwa hivyo, hiki ni kiwango kikubwa sana ambacho sisi hatuna budi kuwapongeza wafanyakazi wetu kwa kuonyesha juhudi zao. Katika pesa hizo zilizopatikana ni asilimia 49 tu ya wapangaji ambao wamelipwa mpaka sasa hivi kwa kiwango hicho. Kati ya wapangaji wetu ambao ni 2167 ni wapangaji 1063 waliokuwa washalipa kiwango hicho mpaka Machi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, nichukue fursa hii tena kumpongeza sana kwa jitihada kubwa anazozifanya za kutembelea katika maeneo yale. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri nina swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa nyumba za Kilimani zina *drainage* mbaya na kusababisha kupatikana maradhi wakati wowote. Je, ni lini watakarabati *drainage* ile.

b) Mhe. Waziri, kwa kuwa nyumba zile zina kero kubwa kwa wananchi wale, ni lini mimi na wewe tutafanya ziara ili kujionea mwenyewe matokeo mabovu ya wananchi wanaoishi katika nyumba zile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba majumba ya Kilimani yapo kwenye hali mbaya na katika majumba yale sisi tuna *flat* 14 tu yaliyobakia yote wananchi wamepewa baada ya kulipwa fidia sehemuambazo nyumba zao zimebomolewa. Tulikwenda juzi na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi tukajionea wenyewe hali halisi ya yale majengo na hivi sasa tumeanzisha mpango maalum wa kuhakikisha kwamba tunafanya ukarabati kwa kutumia *Act* ya *condominium* ambayo inaturuhusu kufanya marekebisho ya mitaro na zile nyumba. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi, namwambia kwamba hiyo ziara tutaifanya na sisi tuko katika harakati kuhakikisha kwamba zile nyumba zimefanyiwa ukarabati. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini kabla ya kuuliza swali langu naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na yaufatiliaji, namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie nguvu zaidi aweze kuendelea vizuri. Baada ya utangulizi huo niipongeze na serikali kwa kuanzisha Shirika la Nyumba ambalo linawezakuwa ni mkombozi kwa mahitaji ya nyumba Zanzibar. Mhe. Spika, pamoja na kwamba shirika hili lina nyumba sasa hivi na zaidi kwenye Mji Mkongwe.

Je, shirika lina mpango gani wa kuchukua maeneo nje ya Mji au Kiwilaya kwa kujenga nyumba na kuwakodisha watu ambao sio lazima waje wakae Shangani, Michenzani au Mji Mkongwe.

Je, serikali mfano huku Wilaya ya Kusini wana mpango, Magharibi "A" wanao mpango huo au na maeneo mengine kwa sababu maeneo bado yapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, ni kweli kabisa hivi sasa shirika lina mpango kwanza kuhakikisha majengo yake wanayafanyia ukarabati na vile vile, tuna mpango kabambe tunataka kuufanya kile kinachoitwa Ng'ambu Tuitakayo. Tukitoka Ng'ambo Tuitakayo, vile vile, tuna mpango wa kuangalia maeneo ambayo yatakuwa yanaweza wawekezaji wetu kuja kushirikiana na sisi katika kujenga nyumba nyengine. Mfano mzuri sasa hivi *Bakhresa Company* wameanza mpango huo wa kujenga nyumba Fumba na sisi tutatafuta maeneomengine ambayo yanauzika kirahisi ili tupate

kujenga nyumba hizo na kuwaondoshea wananchi wetu kero ya kukaa na kusongamana hapa Mjini.

Mhe. Spika, mwisho kabisa napenda kumshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa ushauri wake naahidi kwamba tutaufanyia kazi kwa maslahi ya nchi yetu na vizazi vyetu vya hivi sasa na vijavyo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, maswali yamekwisha na wakati wa maswali umekwisha. Kwanza nina matangazo ya wageni, wageni wetu wa leo tarehe 22/09/2016 ni walimu na wanafunzi kutoka Skuli ya Sekondari ya FLORIAN, Karatu Mkoa wa Arusha. Wenyeji wao ni Skuli ya Ben-bella jumla yao ni wanafunzi 30, msafara huo unaongozwa na Mwalimu John Isarara na Mwalimu Victor Tadei Clement wote kwa pamoja tunawakaribisha naomba mnyanyuke ili waheshimiwa waweze kuwaona. Karibuni sana kwenye Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo jengine ni kwamba tunaomba tukutangazieni kwamba wale waheshimiwa wote ambao hawajarejesha marekebisho ya *C.V* zao wanaombwa waziwasilishe masjala kabla ya tarehe 27 mwezi wa 9. Sasa tatizo lililopo ni kwamba mjumbe ambaye atashindwa kuwasilishwa marekebisho yake kabla ya tarehe hiyo, basi ile taarifa ya awali zilizomo kwenye *C.V* zake ndizo zitakazotumika kwa kazi za kiofisi ikiwa ni pamoja na kuwekwa kwenye tovuti ya Baraza la Wawakilishi. Ahsanteni.

Waheshimiwa Wajumbe, jengine ni ugawaji wa bendera, tunaarifiwa kwamba kutakuwa na zoezi la ugawaji wa bendera kwa ajili ya matumizi yetu leo hii, hivyo basi, Waheshimiwa Wajumbe, tunaombwa tutakapokuwa tunatoka tupitie hapo mapokezi kwa ajili ya kukabidhiwa bendera hizo. Ahsante.

Waheshimiwa Wajumbe, kesho kuna shughuli ya kitaifa ambayo inaongozwa na Mhe. Rais na Waheshimiwa Mawaziri wengi watatakiwa kushiriki kwenye shughuli hiyo, lakini pamoja na sisi ili twende tukaunge mkono hilo jambo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hebu atugaie neno kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kuwa kila tarehe 23 ya mwezi wa 9 kuna shughuli mahsusi kuhusu maamuzi makubwa ya kisera yaliyoamuliwa na wazee wetu waasisi Mapinduzi ya mwaka 1964 kuhusu elimu bila ya malipo. Kutokana na msingi huo Mhe. Spika, wananchi wengi wa Unguja na Pemba wameweza kupata elimu kutokana na sera hiyo, na imeweza kuleta maendeleo makubwa ya nchi

yetu. Kutokana na msingi huo kwa nia na dhamira ya kuendeleza elimu nchini na hususan kwa wale wenzetu wanyonge ambao mara nyingi walishindwa kupata elimu kwa sababu ya uwezo. Lakini kutokana na Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 na sera zake iliweza kwa makusudi kabisa chini ya uongozi mahiri wa mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alitangaza rasmi kwamba elimu iwe bila ya malipo kwa wananchi wote.

Katika kuhakikisha kwamba tunaitekeleza ilivyo adhma hiyo na kuiheshimu siku hiyo, na kwa kuwa nia na dhamira ni kuimarisha elimu nchini, kwa hiyo, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kwa makusudi siku ya kesho kuifanya siku kubwa ya uzinduzi rasmi kwa kusherehekea kutoa elimu bila ya malipo. Kwa hivyo, kwa kuwa Mawaziri na Wajumbe wa Baraza lako tukufu watakuwa na nafasi yakwenda kushiriki katika shughuli hiyo, hivyo, naliomba Baraza lako liahirishe kesho isiwe siku ya shughuli na badala yake shughuli kama hiyo tuifanye siku ya Jumamosi ili tuweze kuendelea na shughuli nyengine za Baraza.

Kwa hivyo, ningeomba kutoa wito kwa Wajumbe wa Baraza tuweke kanuni kando ili tuahirishe shughuli zetu kwa kesho zisifanyike na badala yake zifanyike siku ya Jumamosi tuendelee kama ambavyoMhe.Spika, utatuelekeza. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sasa mimi kazi yangu hapa itakuwa ni kuwahoji ili siku ya kesho tusiitumie na badala yake tuje hapa siku ya Jumamosi ili kuweka kando kanuni. Waheshimiwa, sasa nitawahoji wale wote ambao wanaiunga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili, wanyanyue mikono yao, wale wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

TAARIFA

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kabisa naomba Baraza lako tukufu linikubalie hoja yangu ya kwamba sasa hivi kuna hoja ya serikali kuhusu Mswada wa Marekebisho ya Katiba na pamoja na kwamba kuna vifungu vichache sana vinataka kurekebishwa, lakini suala la Katiba ni suala zito na pamoja na kwamba toleo hili limetoka muda mrefu kidogo uliopita, lakini kwa bahati mbaya sana inawezekana kwa sababu za hapa na pale ikawa umechelewa kutufika sisi. Sasa mswada tumeupata jana

tumeshindwa kupata nafasi ya kuweza kukaa na kujadili na kushauriana na wananchi wetu mbali mbali, na jana kwa kweli tuliondoka muda kama uliouona. Sasa nilikuwa naomba tu Mhe. Spika, nikubalie hoja yangu na naomba wajumbe wairidhie kwamba mswada huu leo tusiujadili na kama kuna shughuli nyengine ulizozipanga tuendelee, lakini kama hakuna, naomba kwamba tupate muda ili tukaupitie ili uje usomwe siku nyengine. Mhe. Spika, naomba kwa ridhaa yako na Baraza zima inikubalie kwamba leo mswada huu tuahirishe, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Hamza, hoja yako nimeisikia na bahati nzuri sana na serikali nayo pia imesikia, kabla sijawahoji kuhusiana na hoja yako nitaomba sasa kupata maelekezo ya serikali kwenye hoja ambayo ameitoa Mhe. Hamza, baada ya hapo nitahoji Waheshimiwa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, tumemsikia Mhe. Hamza, hoja yake aliyotoa na kama ambavyo amesema mswada huu ni kweli ulichapishwa tarehe 30 na ulitimiza yale masharti ya kanuni, lakini kwa vile wajumbe umechelewa kutolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe na wajumbe wameomba wapewe muda zaidi yakwenda kupitia. Pamoja na kwamba vifungu vyenyewe ni viwili lakini unapobadilisha Katiba inabidi pia na wajumbe nao wajiridhishe vizuri. Sasa sisi tunakubaliana na hoja ambayo imetolewa na Mhe. Hamza na tuahirishe leo.

Mhe. Spika: Baada ya maelezo hayo kutoka serikalini, sasa Waheshimiwa Wajumbe nitawahoji kuhusiana na hoja ambayo imetolewa na Mhe. Hamza, wale wote wanaoiunga mkono hiyo hoja kwamba leo tuahirishe ili kuweza kwenda kujiridhisha Waheshimiwa muweze kupitia kwa undani zaidi suala liloletwa mbele yetu la Katiba wanyanyue mikono juu, wanaokataa, waliokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimwia Wajumbe, kwa kuwa shughuli kwenye *order paper* zitakuwa zimekwisha kwa siku ya leo baada ya kuahirisha kwa hiyo hoja ya mabadiliko ya Katiba, naomba kuahirisha Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumamosi saa 3:00 asubuhi.

(Saa 4:28 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi
tarehe 24/09/2016 saa 3:00 asubuhi)